

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA KILOLO



Kumb. Na. KDC/AB/41/01

20/02/2018

TANGAZO LA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo amepokea Kibali cha Ajira chenye Kumb Na: FA/71/363/01/38 cha tarehe 31/07/2017 pamoja na Kibali Kumb. Na: FA/170/363/01/48 cha tarehe 22/09/2017. Aidha kufuatia vibali hivyo Mkurugenzi Mtendaji (W) anawatangazia watanzania wote wenye sifa za kujaza nafasi za kazi kama ifuatavyo:-

1. KAZI: MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA II (Nafasi 1)

SIFA ZA MWOMBAJI

Awe amehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Atakuwa Katibu wa Kamati/Mikutano ya Kijiji
- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Ataratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kutatafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali.
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA NA MSHAHARA WA KUANZIA

TGS C1 = TSHS.525,000/= Hadi Tshs. 668,000

2. KAZI: MTENDAJI WA KIJIJI DARAJA III (Nafasi 9)

SIFA ZA MWOMBaji

Awe amehitimu mafunzo ya Astashahada/Cheti katika mojawapo ya fani zifuatazo: Utawala, Sheria, Elimu ya Jamii, Maendeleo ya Jamii na Sayansi ya Sanaa kutoka katika Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo Dodoma au Chuo chochote kinachotambulika na Serikali.

MAJUKUMU YA KAZI

- Afisa Masuuli na Mtendaji Mkuu wa Serikali ya Kijiji
- Atakuwa Katibu wa Kamati/Mikutano ya Kijiji
- Atakuwa mlinzi wa Amani na Msimamizi wa Utawala Bora katika Kijiji
- Ataratibu na kusimamia upangaji wa utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Kijiji
- Kutatafsiri na kusimamia Sera, Sheria na Taratibu
- Kuandaa taarifa za utekelezaji wa kazi katika eneo lake na kuhamasisha wananchi katika kuandaa na kutekeleza mikakati ya kuondoa njaa, umaskini na kuongeza uzalishaji mali,
- Kiongozi wa wakuu wa vitengo vya kitaalam katika kijiji
- Kusimamia, kukusanya na kuhifadhi kumbukumbu zote na nyaraka za kijiji.

NGAZI YA MSHAHARA NA MSHAHARA WA KUANZIA

TGS B1 = TSHS.390,000/= Hadi Tshs. 489,000/=

3. KAZI: DEREVA DARAJA LA II (Nafasi 5)

SIFA ZA MWOMBaji:

- Awe amehitimu kidato cha nne (iv)
- Awe na Leseni Daraja E Au C1 ambayo ameifanya kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria Mafunzo ya Msingi ya Uendeshaji Magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundı Stadi (VETA) au Chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye Cheti cha Majaribio ya Ufundı Daraja la 11 wafafikiriwa kwanza.

MAJUKUMU YA KAZI

- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari
- Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari.
- Kufanya matengenezo madogomadogo ya gari
- Kufanya usafi wa gari, na
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Msimamizi wake

NGAZI YA MSHAHARA NA MSHAHARA WA KUANZIA

TGS B1 = TSHS.390,000/= Hadi Tshs. 489,000


MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA KWA MWOMBaji:

- Mwombaji awe Raia wa Tanzania
- Mwombaji awe na umri kati ya miaka 18 hadi 45
- Barua zote ziandikwe kwa mkono na ziambatanishwe na nyaraka zifuatazo:
 - Maelezo Binafsi (CV)
 - Nakala za vyeti vya kidato cha nne au sita, cheti cha kuzaliwa na vyeti vya Elimu na taaluma.
 - Picha ndogo mbili (passport size) za hivi karibuni
- Transcript "Testimonial" Provisional Result au Statement of Result havitakubaliwa.
- Mwisho wa kupokea maombi ni **tarehe 09/03/2018 Saa 9:30 Alasiri.**
- Maombi yatakayoletwa baada ya muda uliowekwa katika tangazo hayatapokelewa.
- Tangazo hili linapatikana kuititia Tovuti ya Halmashari; www.kilolodc.go.tz

Barua zote zitumwe kwa:

Mkurugenzi Mtendaji (W)
Halmashauri ya Wilaya ya Kilolo,
S.L.P 2324
KILOLO.

Tangazo hili limetolewa na:



Aloyce Kwezi
Mkurugenzi Mtendaji (W)
KILOLO.